

# Ankara yako ya intaneti inaweza kuongezeka kwa \$30 Mei hii

Hivi karibuni Bunge linaweza kutamatisha Mpango wa Muunganisho wa Gharama Nafuu (ACP).



## UNACHOPASWA KUJUA:

- Maombi na uandikishaji wa ACP hauchakatwi tena kuanzia Februari 8, 2024.
- Kaya ambazo zimeomba, zimeidhinishwa na zinapokea punguzo la kila mwezi la intaneti kabla ya Februari 8, 2024 zitaendelea kupokea manufaa yao ya ACP hadi fedha za ACP zitakapoisha, ilimradi tu kaya iendelee kuwa imesajiliwa kwenye mpango.
- Baada ya fedha za ACP kuisha (zinazotarajiwa Aprili 2024), kaya zinazoshiriki katika ACP hazitapokea tena punguzo la ACP.

## HII INAMAANISHA NINI KWAKO?

Jiandae na ongezeko la ankara yako ya intaneti.

Una machaguo yafuatayo ya kupunguza athari:

- Usichukue hatua yoyote na endelea na huduma yako ya intaneti iliyopo, lakini jiandae kulipa \$30 zaidi kila mwezi.
- Piga simu kwa mtoa huduma wako wa intaneti ili uombe mpango wa bei nafuu. Baadhi wanatoa mipango maalum ya "gharama nafuu" kwa watu ambao wanastahiki ACP.
- Kumbuka kwamba una haki ya kubadilisha au kufuta mpango wako wa huduma ya intaneti ya punguzo la ACP bila adhabu.
- Jiandikishe katika mpango wa serikali kuu wa Lifeline kama bado haushiriki.

## JE, MANUFAA YANGU YA ACP YATADUMU KWA MUDA GANI?

Punguzo lako la ACP litaendelea hadi Aprili. Kuanzia Mei, utaona ongezeko la ankara

## NANI ATAWASILIANA NAMI?

**Mtoa huduma wako atatuma taarifa tatu:**

ya kwanza alipaswa kuwasili kabla Jan. 25, 2024; ya pili inafuata tangazo la FCC la mwezi wa mwisho wa ACP kwa siku 14, na la tatu linaambatana na mzunguko wa mwisho wa ankara kwa kutumia manufaa yote ya ACP kabla ya mpango kuisha

**Notificatons watakuambia:**

- Jinsi ankara yako itakavyobadilika bila punguzo la ACP.
- Tarehe ya ankara ya mwisho ambayo itajumuisha punguzo la ACP.
- Jinsi unavyoweza kubadilisha mipango, kuhamisha kwenda kwa mtoa huduma tofauti au kufuta huduma yako bila adhabu wakati ACP inamalizika.

## KWA MSAADA NA TAARIFA ZAIDI:

Kuwasilisha malalamiko, piga simu:  
888-CALL-FCC (888-225-5322)

Jisikie huru kuwasiliana na Dallas County Connects Hotline kwa 469-946-9491 kwa maswali yoyote au masuala yanayohusiana na ACP Wind-Down.



# Maswali Yanayoulizwa Sana

## **Je, ni mahitaji gani ya ulinzi wa watumiaji kwa Watoa Huduma za Intaneti (ISP) wanaoshiriki katika Mpango wa Muunganisho wa Gharama Nafuu (ACP) wakati wa awamu yake ya mwisho?**

ISP lazima wafuate mahitaji ya ulinzi wa watumiaji hata wakati wa awamu ya mwisho wa ACP. Hii inajumuisha kujiepusha na vitendo au shughuli zisizo za haki na zisizofaa ambazo zinaweza kudhoofisha madhumuni, dhamira au uadilifu wa ACP. Matakwa haya yanalenga kuwalinda watumiaji dhidi ya madhara ya kifedha na kuhakikisha kuwa kaya zinazostahiki hazikabiliwi na mizigo ya ziada ya kifedha.

## **Je, mahitaji ya ulinzi wa watumiaji yataendelea kutumika baada ya wateja kukoma kupokea manufaa ya ACP?**

Ndiyo, baadhi ya mahitaji ya ulinzi wa watumiaji yataendelea kutumika hata baada ya wateja kuacha kupokea manufaa ya ACP. Hii ni kuhakikisha kwamba kaya zinazostahiki hazibebeshwi mzigo wa ziada wa kifedha na kwamba Watoa Huduma za Intaneti (ISP) wanatimiza wajibu wao kwa watumiaji.

## **Je, ISP wanaweza kupunguza mzigo wa kifedha kwa watumiaji baada ya kutamatika kwa ACP?**

Ndiyo, ISP wanaweza kusaidia kuwapunguzia mizigo ya ziada ya kifedha watumiaji baada ya kutamatika kwa ACP kwa kutoa mipango ya huduma ya intaneti ya gharama nafuu iliyoundwa mahsusi kwa ajili ya watumiaji wa kipato cha chini au kwa kuwahamisha wateja kuja kwenye mipango iliyopo ya gharama nafuu. Hii inalenga kuzisaidia kaya kuendelea kupata intaneti ya gharama nafuu.

## **Nini kitatokea iwapo kaya inayostahiki itashindwa kulipa gharama za huduma inayotegemea ACP?**

Kwa mujibu wa kanuni za ACP, ISP wanaoshiriki haziwezi kusitisha huduma ya kaya inayotegemea ACP kwa sababu ya kutolipa hadi siku 90 zipite tangu tarehe ya malipo ya anbara. ISP wanaruhusiwa kuzihamishia kaya kwenye mpango wa gharama nafuu iwapo wataingia katika hali ya kutowajibika baada ya tarehe inayotakiwa, na taarifa ya mapema kwa kaya.

## **Je, ada za kutamatisha mipango ya huduma mapema zinazotumika kwa kaya zinazostahiki zinazokatisha mipango ya huduma kulingana na mikataba ya huduma iliyoongezwa baada ya ACP kuisha?**

Hapana, ISP hawawezi kutoza ada za kusitisha mapema huduma kwa kaya zinazostahiki ambazo hukatisha mipango ya huduma kwa kutegemea mikataba ya huduma iliyoongezwa hata baada ya ACP kuisha. Hii inalinda kaya dhidi ya adhabu za kifedha kwa kusitisha mikataba ya huduma mapema, hata kama hazitapokea tena manufaa ya ACP.

## **Je, ISP wanakatazwa vipi kujihusisha na vitendo au shughuli zisizo za haki na zisizo za busara zinazohusiana na ACP?**

ISP hawaruhusiwi kujihusisha na vitendo au shughuli zozote ambazo zinaweza kudhoofisha madhumuni, dhamira au uadilifu wa ACP, hata baada ya kaya kuacha kupokea manufaa ya ACP. Hii ni pamoja na matangazo ya uwongo au ya upotoshaji ya ACP au kujitenda kama wao sio watoa huduma wanaoshiriki katika ACP wakati sivyo. Ukiukaji unaweza kuripotiwa kwa FCC.

## **Je, wateja wanawezaje kuwasilisha malalamiko kuhusu mtoa huduma kutii kanuni na matakwa ya kutamatisha ACP?**

Wateja wenye wasiwasi kuhusu watoa huduma kutii kanuni na matakwa ya kutamatisha ACP wanaweza kuwasilisha malalamiko kwenye Tume kwa kutembelea [ConsumerComplaints.fcc.gov](http://ConsumerComplaints.fcc.gov). Kaya zenye maswali zinaweza kuwasiliana na Kituo cha Msaada cha ACP kwa 877-384-2575 au [acpinfo@fcc.gov](mailto:acpinfo@fcc.gov). Wateja ambao ni Viziwi au Wanasikia kwa Shida wanaweza kutumia Simu ya Moja kwa Moja ya ASL kwa 844-432-2275.